

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI - ZANZIBAR (ZURA)

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar, imeanzishwa chini ya sheria Nam.7/2013 ikiwa na jukumu la kusimamia huduma za Maji na Nishati hapa Zanzibar.

ZURA kwa uwezo na Mamlaka iliyonayo chini ya kifungu nambari 16 (C) ya sheria Nam. 7/2013 inapenda kuwatangazia wananchi wenye sifa kujaza nafasi za ajira kama zifuatazo katika Afisi zake za Unguja na Pemba.

1. MTAKWIMU DARAJA LA II. Nafasi 1 Unguja,

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari
- Shahada ya kwanza/Stashahada ya juu au Stashahada ya Uzamili katika fani ya Takwimu, Hisabati au fani inayolingana kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.
- Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada.

2. KARANI MASJALA DARAJA LA III. Nafasi 2 Unguja,

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari
- Awe Stashahada ya kawaida ya Kutunza kumbukumbu au fani inayolingana na hiyo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikalini ya Mapinduzi Zanzibar.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.
- Awe uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada.

3. MWANGALIZI WA AFISI DARAJA LA III. Nafasi 1 Unguja

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari
- Awe Stashahada ya Utawala, au fani inayolingana na hiyo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikalini ya Mapinduzi Zanzibar
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.
- Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziadi

4. MAPOKEZI DARAJA LA III. Nafasi 2 Unguja

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari
- Awe na Stashahada ya mapokezi, au fani inayolingana na hiyo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikalini ya Mapinduzi Zanzibar
- Awe na uwezo wa kuzungumza na kuandika kwa ufasaha Lugha ya Kiswahili na Kingereza.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.
- Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada.

5. TAARISHI/ MUHUDUMU DARAJA LA III Nafasi 2 Unguja

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari
- Awe na cheti cha kidato cha Nne (F.IV) kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada.

6. KATIBU MUHTASI DARAJA LA III. Nafasi 2 Unguja.

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari
- Awe Stashahada ya fani ya Uhazili kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.
- Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada.

TAARIFA ZA JUMLA

Kwa waombaji wote watakaopata bahati ya kuchaguliwa kutafanyika usaili katika ofisi za ZURA zilizopo Maisara Zanzibar.

Muombaji yeyote atakaechaguliwa anatakiwa awe tayari kufanya kazi katika Afisi yoyote ya ZURA.

TAREHE YA MWISHO WA MAOMBI

Maombi yataanza kupokelewa kuanzia leo tarehe 14/08/2019 na tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 21/08/2019.

NAMNA YA KUWASILISHA MAOMBI

Waombaji wote wanatakiwa kuwasilisha barua ya maombi iliyoandikwa kwa mkono katika ofisi za ZURA na kuambatanisha na vivuli vya taarifa zifuatazo;

1. Vivuli vya Vyeti vya kumalizia masomo
2. Maelezo Binafsi (CV)
3. Cheti cha kuzaliwa
4. Picha mbili za paspoti zilizopigwa karibuni
5. Kitambulisho cha Mzanzibari

Maombi yote yawasilishwe katika anuani ifuatayo;

MKURUGENZI MKUU,

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI (ZURA)

S.L.P 2238, GHOROFA YA PILI, JENGO LA MFUKO WA BARABARA

MAISARA

ZANZIBAR

**KWA WALE WALIOKO PEMBA MAOMBI YA YAPELEKWE AFISI ZA ZURA
AFISI ZA SERIKALI GOMBANI - PEMBA.**

ANGALIZO:

**MAELEZO ZAIDI KUHUSIANA NA TANGAZO HILI FUATILIA KATIKA TOVUTI
YA MAMLAKA www.zura.go.tz, NA GAZETI LA ZANZIBAR LEO LA TAREHE
15/08/2019.**

